**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**(MASJALA YA WILAYA MTWARA)**

**MTWARA**

**RUFA YA ARDHI NA. 26 YA 2021**

**CAROLINA BENEDICT NAMADENGWA.........................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ALLY SALUM NDAVA.....................................................MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**

**MURUKE, J.**

Bi. Carolina Benedict Namadengwa (mama mkulima) alimuuzia bwana Ally Salum Ndava eneo la kujenga kibanda cha biashara kwa thamani ya shilingi laki saba tarehe 27 mwezi wa nane 2016. Makubaliano hayo yaliwekwa kwenye maandishi. Bi Carolina anadai bwana Ally Salum Ndava amekataa kurudisha eneo lingine la pili walilokubaliana akae kwa muda baada ya kuliendeleza.

Kufuatia ubishi huo, Bi Carolina alifungua kesi katika baraza la Ardhi. Baada ya kusikilizwa pande zote, Baraza la Kata la Luagala - Tandahimba lilimtamka Ally Salum Ndava kuwa mmiliki halali wa eneo bishaniwa. Bi Carolina hakuridhika na uamuzi wa baraza la Ardhi la Kata, akafungua rufaa katika baraza la Ardhi Mkoa wa Mtwara. Baada ya kusikilizwa pande zote mbili, Baraza la Ardhi la rufaa lilitupilia mbali rufaa, na kukubaliana na uamuzi wa baraza la kata kuwa mrufaniwa Ally Salum Ndava ndiye mmiliki halali wa eneo bishaniwa.

Uamuzi ulipingwa na Bi. Carolina aliyefungua rufaa hii, aliorodhesha saba sababu. Siku ya kusikilizwa, Mrufani alioomba sababu zake za rufaa zipokelewe kama maelezo ya kina ya kuunga mkono rufaa. Vile vile mrufaniwa naye aliomba majibu ya sababu za rufaa zipokelewe kama maelezo ya kina ya kubeza rufaa. Maombi hayo yalikubalika na Mahakama.

Baada ya kupitia kumbukumbu za baraza la kata, na nyaraka zote, nimegundua kuwa, kuna hati mbili za mauziano ambazo zinahusu eneo bishaniwa, zinatofautiana kwa kiwango kikubwa kwenye makubaliano pamoja na kwamba wahusika ni wale wale, na tarehe ni moja. Kwa uhakika wa rejea, makubaliano ya kwanza yanayotambuliaka na mrufani yanasomeka hivi

**HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA**

**AFISA MTENDAJI KATA, KATA YA LUAGALA,**

**S. L. P 03, TANDAHIMBA**

**27/08/2016.**

**KWA YEYOTE ANAEHUSIKA**

**KATA YA LUAGALA**

**YAH: HATI YA MAUZIANO YA KIWANJA CHA UJENZI WA KIBANDA CHA BIASHARA ENEO LA SOKONI KIJIJI CHA LUAGALA**

**WAHUSIKA 1. KAOLINA B. NAMADENGWA – MUUZAJI**

**2. ALLY S. NDAVA – MNUNUZI**

**Watajwa hapo juu ni wakazi wa Kijiji cha Luagala kilichopo kata ya Luagala leo tarehe 27/08/2016 mbele ya ofisi ya Kata. Wamekubaliana kuuziana kiwanja cha ujenzi wa kibanda cha Biashara kwa**

thamani ya Tshs 700,000. Eneo lipo katikati ya kijiji cha Luagala njia panda. Pesa hizo zitalipwa tarehe 12/09/2016 siku ya Jumatatu hati hii ni Makubaliano ya ndugu watajwa hapo juu mbele yangu mimi Afisa Mtendaji kata, Musa H. Cheusi.

SAHIHI ZA WAHUSIKA

1. KALOLINA B. NAMADENGWA AMESAINI
2. ALLY S. NDAVA AMESAINI

MASHAHIDI

1. FADHILI HAMISI JUMA AMESAINI
2. DADI MCHINDO MZEE (MTASHONA) AMESAINI

AMESAINI
WEO LUAGALA

Kwa upande mwingine bwana Ally Salum Ndava, hayatambui makubaliano hayo hapo juu bali anakubaliana na haya hapa chini.

OFISI YA MTENDAJI KATA, S.L.P 03,

LUAGALA, TANDAHIMBA

27/08/2016

YEYOTE ANAYEHUSIKA

YAH; HATI YA KUUZA ENEO LA KUJENGA KIBANDA CHA BIASHARA

Bi. Karolina B. Namadengwa (mama mkulima) mkazi wa kijiji cha Luagala amemuuzia eneo la kujenga kibanda cha biashara ndugu Ally S. Ndava mkazi wa kijiji chaChaume. Eneo hilo amemuuzia kwa thamani Tshs 700,000/= (laki saba). Eneo lipo jirani na nyumba yam zee Litanda na panapoanzia barabara ya kwenda kijiji cha Chidede. Pesa hizo zimelipwa zote kupitia ofisi hii leo tarehe 27/08/2016 mbele ya ushuhuda wa watu wafuatao.

1. BI KAROLINA B. NAMADEGWA sahihi ya muuzaji .amesaini
2. NDUGU ALLY S. NDAVA sahihi ya mnunuzi amesaini
3. NDUGU FADHILI S. JUMA sahihi ya shahidi wa muuzaji amesaini

4. **NDUGU DADI. M. MZEE (Mtashona) sahihi ya shahidi wa mnunuzi amesaini.**

**Ahsante**

Kwa hali ilivyo, kila upande unakataa, makubaliano ya mwenzake. Mahakama hii inashangaa na kujiuliza nikielelezo kipi kilifuatwa na Mabaraza yote mawili, kufikia uamuzi wa kumpa haki bwana Ally Salum Ndava. Kwa vyovyote vile, ushahidi wa nyaraka hizi mbili tofauti zinazohusu makubaliano ya kuuziana kipande cha ardhi yanatakiwa yatathiminiwe na Baraza lililosikilizwa shauri na kupongea ushahidi. Ili kutenda haki hukumu na mwenendo wa Baraza la Ardhi la Kata umefutwa na amri zote kuwekwa pembeni. Vile vile hukumu ya Baraza la Ardhi la Mkoa nayo imefutwa. Na enaelekezwa kuwa kesi ikaanze upya katika Baraza la Ardhi la Kata ndani ya siku sitini (60) kuanzia tarehe 01/08/2022. Sehemu inayobishaniwa baina ya Bi Carolina Benedict Namadengwa na Ally Salum Ndava izisiendelezwe na yoyote mpaka mgogoro utakapo amuliwa na Baraza la Ardhi la Kata.

**Z. G. Muruke**

**Jaji**

**20/07/2022**

Uamuzi huu umesomwa na kutolewa mbele ya Mrufani na Mfuraniwa wakiwa wanajiwakilisha wenyewe.

**Z. G. Muruke**

**Jaji**

**20/07/2022**